# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

## MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU MAELEZO

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

3. Kuanzishwa kwa Wakala.

4. Jina fupi, Muhuri na Nembo ya Wakala.

5. Malengo ya Wakala.

6. Kazi za Wakala.

### SEHEMU YA TATU
### UONGOZI NA USIMAMIZI WA WAKALA

7. Uanzishwaji wa Bodi.

8. Uteuzi na sifa za Mwenyekiti.

9. Kazi za Bodi.

10. Kukasimu kazi za Bodi.

11. Mgongano wa maslahi.

12. Mualikwa.

13. Kumsitisha au kumsimamisha mjumbe wa Bodi.

14. Kamati za Bodi.

15. Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

16. Katibu wa Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MTENDAJI NA WAFANYAKAZI WENGINE WA WAKALA

17. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

18. Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

19. Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

20. Wafanyakazi wa Wakala.

21. Idara na Vitengo vya Wakala.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

22. Fedha na vyanzo vya mapato ya Wakala.

23. Kubakiza Fedha.

24. Bajeti.

25. Kufungua hesabu ya benki.

26. Hesabu na ukaguzi.

27. Ripoti ya mwaka.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

28. Makosa na Adhabu.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

29. Kuhaulisha mali na madeni.

30. Kinga.

31. Kanuni.

32. Kubakiza.

## JADWELI

SHERIA NAM. 11 YA 2019

NIMESAINI

{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

31 Disemba, 2019

# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Barabara Zanzibar, 2019 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Barabara Zanzibar uliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 (1) cha Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Ushauri ya Wakala iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7 (1) cha Sheria hii;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii na inajumuisha mtu mwengine anayefanya kazi za Mwenyekiti;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 17 cha Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi za Zanzibar;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya barabara;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

"Barabara za Umma" ina maana kama ilivyoainishwa chini ya kifungu cha 2 cha Sheria ya Barabara Sura ya 134;

"Huduma za barabara" inajumuisha madaraja, alama za barabarani na miundombinu yoyote iliyopo au inayokatisha barabara za umma;

"Matengenezo ya barabara" maana yake ni kazi zote zinazohusu utunzaji na uimarishaji wa barabara;

"Mtandao wa Barabara" maana yake ni mtandao wa barabara zote za Zanzibar;

"Barabara" ina maana kama iiivyoainishwa chini ya kifungu cha 2 cha Sheria ya Barabara Sura ya 134;

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Wakala.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Wakala wa Serikali utakaojulikana kama Wakala wa Barabara Zanzibar.

(2) Wakala utakuwa ni chombo cha Serikali unaojitegemea kwa baadhi ya mambo, na kwa idhini ya Waziri, utakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kumiliki, kununua au kuhamisha mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia kwenye mkataba au muamala wowote kwa kuzingatia sheria zilizopo;

(c) kukopa fedha kutoka katika Taasisi yoyote ya fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(d) kufanya au kutekeleza jambo au kitu chochote ambacho, Wakala kwa asili yake, unaruhusika kufanya au kutekeleza kwa mujibu wa sheria.

Jina fupi, Muhuri na Nembo ya Wakala.

**4.**-(1) Kutakuwa na jina fupi, muhuri na nembo ya Wakala katika umbo na ukubwa kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya jina fupi, muhuri na nembo ya Wakala kwa waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mtendaji au afisa yeyote wa Wakala aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji.

(3) Waraka wowote ili uwe ni hati iliyotolewa na Wakala, utatakiwa kuwekwa muhuri wa Wakala na kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Wakala.

**5.** Malengo ya Wakala yatakuwa ni:

(a) kuhakikisha Zanzibar ina mtandao wa barabara wa kisasa ambao una ubora, salama na wenye kuridhisha na kushajihisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi Zanzibar;

(b) kuhakikisha Wakala una wataalamu mahiri wa barabara wa kutosha na wa kudumu; na

(c) kuhakikisha huduma za barabara zinawafikia wananchi kwa ukaribu.

Kazi za Wakala.

**6.** Kazi za Wakala zitakuwa ni:

(a) kujenga barabara mpya na kuzifanyia matengenezo barabara zilizopo kwenye mtandao wa barabara;

(b) kuwasimamia wataalamu ambao wanajenga barabara;

(c) kutayarisha na kutekeleza mipango ya muda mfupi na mrefu ya matengenezo ya barabara;

(d) kuendeleza, kuhifadhi na kuweka mifumo ya usimamizi wa utunzaji wa barabara kulingana na wakati uliopo;

(e) kupanga, kusanifu na kuendeleza barabara zote za Zanzibar ili kuhakikisha kwamba barabara zinakuwa katika hali nzuri na zenye ubora wakati wote;

(f) kufanya utafiti kwa kushirikiana na taasisi yoyote kwa lengo la kurahisisha mipango, uendelezaji na matengenezo ya barabara;

(g) kuanzisha, kuendeleza na kulinda mfumo wa udhibiti wa uzito wa gari kwa ajili ya kudhibiti matumizi mabaya ya barabara ili kuwa na barabara endelevu;

(h) kumshauri Waziri kuhusiana na masuala yote ya barabara;

(i) kutayarisha miongozo, viwango vya usanifu na vigezo vya kazi za barabara na kusimamia utekelezaji wake;

(j) kuthibitisha michoro na usanifu na kuhakikisha barabara zinajengwa kwa mujibu wa viwango vya usanifu na ubora;

(k) kuendeleza na kuwajengea uwezo sekta za barabara ukijumuisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uendelezaji, uhifadhi na utunzaji wa barabara;

(l) kusimamia na kudhibiti shughuli za ujenzi na matengenezo ya barabara zikiwemo usalama wa barabara na masuala ya kimazingira;

(m) kusimamia na kudhibiti uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara;

(n) kushirikiana na mamlaka za usalama barabarani juu ya mambo yanayohusu usalama wa watu na wanyama kwenye barabara za umma; na

(o) kutekeleza kazi nyengine zozote ambazo imepewa na Waziri au ambazo ni muhimu kwa ajili ya kufikia malengo ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI NA USIMAMIZI WA WAKALA

Uanzishwaji wa Bodi.

**7.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Ushauri ya Wakala ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar;

(c) Mkurugenzi Mtendaji;

(d) Mkurugenzi anayehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(e) Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Barabara, Zanzibar;

(f) Mwanasheria wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(g) Mhandisi mmoja kutoka chama cha uhandisi kilichosajiliwa.

(2) Isipokuwa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watachaguliwa na Waziri kwa kushirikiana na taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, taaluma na jinsia.

(3) Masharti yanayohusiana na muda wa utumishi wa wajumbe, akidi, maamuzi ya vikao na taratibu nyengine za Bodi zitaainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

(4) Waziri anaweza, kila baada ya muda, kurekebisha Jadweli endapo itahitajika.

Uteuzi na Sifa za Mwenyekiti.

**8.**-(1) Kutakuwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kama Mwenyekiti wa Bodi ikiwa:

(a) ni mzanzibari;

(b) mwenye angalau shahada ya kwanza katika fani ya uhandisi, sheria, usimamizi wa umma, utumishi wa umma au fani nyengine yoyote inayofanana na hizo kutoka katika taasisi inayotambulika;

(c) mwenye uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi (10) katika utumishi wa umma; na

(d) mwenye kiwango cha juu cha uweledi katika kutekeleza mambo ya Wakala kwa ufanisi na ubora.

Kazi za Bodi.

**9.** Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kumshauri Waziri katika mambo yanayohusiana na:

(i) sera na mikakati ya barabara;

(ii) uandaaji na upitiaji wa mipango ya utekelezaji, bajeti, ripoti na taarifa za ukaguzi;

(iii) utekelezaji wa:

(a) mpango mkakati wa Wakala;

(b) mpango wa mwaka wa Wakala;

(c) mpango wa ununuzi wa Wakala; na

(d) makubaliano yoyote ya utekelezaji;

(b) kupendekeza muundo wa kitaasisi, muundo wa mishahara ya wafanyakazi na maslahi mengineyo kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(c) kupendekeza kuhusu uanzishaji wa idara, vitengo au sehemu ndani ya Wakala kwa mujibu wa muundo wa Wakala ulioidhinishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma; na

(d) kufanya kazi nyengine zozote zilizoainishwa na Sheria hii au ambazo ni muhimu katika kufikia malengo ya uanzishwaji wa Wakala huu.

Kukasimu kazi za Bodi.

**10.** Bodi inaweza, ikiwa itaona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mkurugenzi Mtendaji, kamati au kwa afisa mwengine yeyote wa Wakala.

Mgongano wa maslahi.

**11.** Mjumbe yeyote ambaye atakuwa na maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo katika mkataba au mkataba unaopendekezwa au jambo lolote linalojadiliwa na Bodi, atatangaza maslahi yake kwa Bodi na hatotakiwa kushiriki katika majadiliano juu ya jambo hilo.

Mualikwa.

**12.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye siyo mjumbe wa Bodi kushiriki katika majadiliano yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu lakini mualikwa huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kumsitisha au kumsimamisha mjumbe wa Bodi.

**13.** Waziri anaweza kumsitisha au kumsimamisha mjumbe yeyote wa Bodi isipokuwa Mwenyekiti na mjumbe anaeingia kwa nafasi yake ikiwa mjumbe huyo:

(a) anashindwa kutekeleza kazi zake za kiofisi;

(b) ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na udanganyifu, kutokuwa muaminifu au kukosa maadili; au

(c) ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi iliyoridhiwa na Mwenyekiti.

Kamati za Bodi.

**14.**-(1) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake, kuanzisha Kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu kama Bodi itakavyoamua.

(2) Utaratibu wa vikao na mambo mengine yanayohusiana na Kamati hizo zitakazoanzishwa utakuwa kama utakavyoainishwa na Bodi.

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

**15.**-(1) Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi ikiwa:

(a) amefariki;

(b) ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi iliyoridhiwa na Mwenyekiti;

(c) atajiuzulu au atakuwa kwa namna yoyote amepoteza sifa za kuwa mjumbe wa Bodi; au

(d) atashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu za kimwili au kiakili.

(2) Kwa kuzingatia masharti yanayohusiana na akidi, Bodi inaweza kuendelea na shughuli zake bila ya kujali kutokuwepo kwa mjumbe yeyote, na kitendo chochote kitakachofanyika katika kikao hicho hakitokosa uhalali kwa sababu tu ya kasoro iliyokuwepo katika uteuzi kuhusiana na mtu aliyekusudiwa kuwa ni mjumbe.

Katibu wa Bodi.

**16.**-(1) Bodi itamteua Mwanasheria anaefaa ambaye ni mfanyakazi wa Wakala kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Katibu atawajibika kwa Bodi na atahakikisha kwamba:

(a) anachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi ambazo zitathibitishwa katika kikao kinachofuata cha Bodi na kuwekwa sahihi na Mwenyekiti wa Kikao na Katibu wa Bodi;

(b) kumbukumbu sahihi na za uhakika za Bodi zinahifadhiwa vizuri;

(c) taarifa sahihi za vikao vya Bodi zinatolewa kwa wajumbe;

(d) anatoa ushauri sahihi kwa Bodi pale inapohitajika; na

(e) anafanya jambo jengine lolote ambalo Bodi inaweza, kila baada ya muda, kumuelekeza.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MTENDAJI NA WAFANYAKAZI WENGINE WA WAKALA

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**17.** Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais.

Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

**18.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya uhandisi au usimamizi wa miradi inayohusiana na barabara kutoka kwenye taasisi inayotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi katika fani ya uhandisi inayohusiana na barabara; na

(d) ana kiwango cha juu cha uweledi katika kutekeleza mambo ya Wakala kwa ufanisi na ubora.

Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

**19.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Wakala na atatekeleza majukumu ya kila siku.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji yatakuwa ni:

(a) kusimamia masuala yote ya kiufundi na ya kitaalamu ya barabara ya Wakala;

(b) kusimamia mapato na matumizi yote ya Wakala kwa mujibu wa Sheria zinazohusika;

(c) kuendesha masuala ya Wakala kwa ufanisi na kwa thamani halisi inayolingana;

(d) kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote wamepatiwa mafunzo yatayowawezesha kutekeleza majukumu yao kitaalamu, kimaadili na kiuwajibikaji;

(e) kusimamia mambo ya kinidhamu kwa wafanyakazi wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(f) kutoa msaada wa kitaalamu kwa Bodi;

(g) kutoa taarifa juu ya shughuli za Wakala kwa Bodi;

(h) kuhakikisha kuwa malengo ya Wakala yanafikiwa;

(i) kusimamia na kuendeleza utendaji wa kazi zote za Wakala kwa:

(i) usimamizi wa utendaji wa kila siku wa Wakala;

(ii) usimamizi wa fedha, mali na shughuli nyengine za Wakala; na

(iii) kufanya jukumu jengine lolote ambalo ni muhimu kwa utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Wafanyakazi wa Wakala.

**20.**-(1) Wakala unaweza, kwa mujibu wa masharti na vigezo, kuajiri wafanyakazi au kukodi mshauri elekezi au mtaalamu kama itakavyoonekana inafaa kwa utekelezaji mzuri wa kazi za Wakala kwa kufuata masharti ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

(2) Uajiri wa wafanyakazi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

(3) Wafanyakazi wote halali waliopo katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara wataendelea kufanyakazi na watachukuliwa kuwa ni wafanyakazi wa Wakala baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Idara na Vitengo vya Wakala.

**21.**-(1) Wakala unaweza kuanzisha idara na vitengo kwa idadi na kwa namna kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakuu wa idara watateuliwa na Waziri kutokana na mapendekezo ya Bodi na wakuu wa vitengo watateuliwa na Bodi baada ya kupendekezwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Wakuu wa idara na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(4)(a) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Wakala utakuwa na Ofisi ndogo ya Pemba ambayo itaongozwa na Mkuu wa Ofisi hiyo ambae atateuliwa na Waziri.

(b) Ofisi ndogo ya Pemba itafanya kazi zake chini ya uangalizi na maelekezo ya Mkurugenzi Mtendaji.

(5) Katika kutekeleza majukumu yake, Waziri atakuwa na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa sera zinazohusiana na Wakala na kutoa maelekezo na maagizo ya jumla kwa Bodi ya Wakala.

(6) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria hii, Wakala utawajibika kuwasilisha taarifa zozote za kiutawala na kiuendeshaji kwa Wizara kila zinapohitajika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na vyanzo vya mapato vya Wakala.

**22.** Fedha na vyanzo vya mapato vya Wakala vitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya matumizi ya Wakala;

(b) fedha zinazotokana na ada au tozo zinazolipwa kwenye Wakala kutokana na utowaji wa huduma zake;

(c) fedha zinazopatikana kutoka Mfuko wa Barabara za matengenezo ya barabara;

(d) ruzuku, msaada au zawadi zitakazopokelewa kutoka katika taasisi au jumuiya yoyote;

(e) fedha zitakazotokana na kukodishwa vifaa vya ujenzi wa barabara; na

(f) fedha nyengine zozote zitakazopatikana kihalali katika utekelezaji wa kazi za Wakala au vyenginevyo.

Kubakiza Fedha.

**23.** Wakala unaweza kubakiza kiwango cha fedha kilichokusanywa kutokana na huduma unazozitowa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Bajeti.

**24.**-(1) Wakala, kabla ya mwaka mpya wa fedha kuanza, utaandaa bajeti ya mwaka na utawasilisha kwa Bodi kwa mazingatio na baada ya hapo utawasilisha kwa Waziri kwa kuzingatia na kuidhinisha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Waziri ataiwasilisha bajeti ya mwaka ya Wakala kwa Baraza la Wawakilishi katika utaratibu na namna ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Kufungua hesabu ya benki.

**25.** Wakala, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, utafungua hesabu ya benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake kwa mujibu wa Sheria hii.

Hesabu na ukaguzi.

**26.**-(1) Wakala utaweka na kuhifadhi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Mkurugenzi Mtendaji, kila mwisho wa mwaka wa fedha, ataandaa au ataagiza kuandaliwa:

(a) taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka huo wa fedha;

(b) taarifa ya mali na madeni ya Wakala hadi kufikia siku ya mwisho ya mwaka wa fedha, ambayo imewasilishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi mwengine atakayeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) taarifa nyengine yoyote ya fedha kama itakavyohitajika kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(3) Nakala za taarifa au ripoti zilizoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, na nakala ya taarifa ya mkaguzi kama ipo, zitawasilishwa kwa Bodi kwa mazingatio na baada ya hapo zitawasilishwa kwa Waziri pamoja na ripoti ya utekelezaji wa kazi za Wakala kwa mwaka huo wa fedha, na baada ya kuzipokea, Waziri ataziwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi.

Ripoti ya mwaka.

**27.**-(1) Wakala, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, utawasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka inayohusiana na mwaka huo na itajumuisha:

(a) nakala za hesabu za Wakala zilizokaguliwa pamoja na ripoti ya mkaguzi inayohusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya utekelezaji dhidi ya malengo muhimu na taarifa nyengine yoyote inayohusiana nayo;

(c) ripoti ya utendaji wa Wakala kwa kipindi hicho cha mwaka wa fedha; na

(d) taarifa nyengine inayohusiana na kazi za Wakala kama Waziri atakavyohitaji.

(2) Waziri atahakikisha kwamba nakala ya ripoti ya mwaka ya Wakala inawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, ndani ya miezi miwili au katika kikao kinachofuta katika Baraza la Wawakilishi baada ya kupokea ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

**SEHEMU YA SITA**
**MAKOSA NA ADHABU**

Makosa na Adhabu.

**28.**-(1) Mtu aliyeajiriwa kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria hii ambaye:

(a) kutokana na nafasi yake ya kazi amepata taarifa yoyote na akaitumia taarifa hiyo kwa maslahi yake binafsi au kwa miamala ya kibiashara ambayo itachochea au kuhatarisha usalama, maslahi au miamala ya kibiashara kwa kupata faida binafsi;

(b) kwa makusudi anashiriki katika jambo au anaharibu taarifa au anatoa taarifa za uongo kwa faida binafsi; na

(c) anakwenda kinyume au anashindwa kufuata sharti lolote la Sheria hii.

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini ya fedha za kitanzania zisizopungua Shilingi Milioni Mbili lakini zisizozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

(2) Mtu ambaye atauza, atatumia au kuruhusu kuuzwa au kutumika malighafi, mashine au chombo chochote cha moto cha Wakala kwa matumizi yake binafsi na bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi Mtendaji, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini ya fedha za kitanzania zisizopungua Shilingi Milioni Tatu lakini zisizozidi Shilingi Milioni Kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitano au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

(3) Mtu au taasisi ambayo itatumia au kuruhusu kutumia jina fupi, muhuri au nembo ya Wakala bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi Mtendaji, itakuwa imetenda kosa na ikipatikana na hatia itawajibika kulipa faini ya fedha za kitanzania zisizopungua Shilingi Milioni Tatu lakini zisizozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

(4) Mtu ambaye atamkatalia au atamzuiya afisa yeyote wa Wakala kutekeleza majukumu yake aliyopewa chini ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini ya fedha za kitanzania zisizopungua Shilingi Milioni Moja lakini zisizozidi Shilingi Milioni Tatu au kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka miwili au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

(5) Mtu ambaye amepewa idhini na akatumia mashine au chombo chochote na kusababisha uharibifu kwa uzembe au kwa kukusudia atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atawajibika kulipa faini ya fedha za kitanzania zisizopungua Shilingi Milioni Tatu lakini zisizozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

Kuhaulisha mali na madeni.

**29.** Mali na madeni ambayo yapo kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kabla ya Sheria hii, mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii yatachukuliwa kuwa yamehaulishwa kwa Wakala chini ya masharti ya Sheria hii.

Kinga.

**30.** Mjumbe wa Bodi au mfanyakazi yeyote aliyeajiriwa na Wakala hatowajibika yeye binafsi kwa jambo lolote au kitu alichokifanya au ameacha kukifanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa kazi zake ndani ya mazingira ya kazi au utekelezaji wa jukumu lake chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**31.-**(1) Waziri anaweza, baada kushauriana na Bodi, kutunga Kanuni kwa utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri atatunga Kanuni kwa kuainisha:

(a) utumiaji, usalama na matengenezo ya barabara zote za Zanzibar;

(b) uwekaji wa miundombinu juu, karibu, pembezoni au chini ya barabara zote za Zanzibar;

(c) ada zitakazotozwa chini ya Sheria hii;

(d) kuondoa, kuvunja au kubadilisha chochote kilichozidi au kuondoa majengo au miti inayozuiya barabara yoyote ya Zanzibar au inayosababisha hatari au usumbufu kwa watumiaji wa barabara; na

(e) jambo lolote ambalo ni muhimu na linahitajika kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Wakala.

Kubakiza.

**32.** Jambo lolote lililofanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litaendelea na litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

---

### UTARATIBU WA VIKAO VYA BODI
**[Chini ya kifungu cha 7(3)]**

---

Vikao vya Bodi.

**1.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja kwa kila kipindi cha miezi mitatu na inaweza kukutana kwa vikao vya dharura muda wowote ikiwa ipo haja ya kufanya hivyo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaitishwa na Mwenyekiti.

(3) Endapo Mwenyekiti atakuwa hayupo, Makamo Mwenyekiti ataitisha mkutano wa Bodi.

(4) Endapo Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti watakuwa hawapo, wajumbe waliopo watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao, na mjumbe aliyechaguliwa atakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti.

Muda wa Wajumbe wa Bodi.

**2.**-(1) Mwenyekiti wa Bodi atatumikia nafasi kwa kipindi cha miaka minne kuanzia tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(2) Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Bodi watatumikia nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Makamo Mwenyekiti.

**3.** Wajumbe wa Bodi watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti wa Bodi.

Akidi ya kikao.

**4.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda akidi ya vikao vya Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

**5.** Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa makubaliano na ikiwa makubaliano hayatofikiwa, maamuzi yatafanyika kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Utaratibu wa vikao.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kujiwekea utaratibu wa uendeshaji wa vikao vyake na mwenendo bora wa shughuli zake ukijumuisha kamati za Bodi.

Maposho ya Wajumbe.

**7.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watapewa maposho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni au Miongozo yake.

Kujiuzulu.

**8.** Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Bodi anaweza, wakati wowote kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa mamlaka ya uteuzi na kutoka tarehe iliyoainishwa katika taarifa au ikiwa tarehe haijaainishwa, kutoka tarehe iliyopelekwa taarifa hiyo kwa mamlaka ya uteuzi, atasita kuwa mjumbe.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 3 Disemba, 2019.

.........................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***